# MATUMIZI YA FASIHI KATIKA UKUZAJI WA STADI YA TAFAKURI TUNDUIZI

***Laurien Tuyishimire***
*Chuo Kikuu cha Rwanda - Rwanda*
*tulaurien@gmail.com*

*na*

***Wallace Kapele Mlaga***
*Chuo Kikuu cha Rwanda - Rwanda*
*wamlaga@gmail.com*

## Ikisiri

*Wanafunzi wa vyuo vikuu hawana kiwango cha juu cha stadi ya tafakuri tunduizi kutokana na kwamba hawakupewa misingi mizuri ya kuendeleleza stadi hii kuanzia shule za sekondari (Saleh, 2019). Kutoka na hali hii, tuliona kuna haja ya kutafiti matumizi ya fasihi katika ukuzaji wa stadi ya tafakuri tunduizi katika shule teule za sekondari nchini Rwanda. Data zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya uchanganuzi wa matini, usaili, na ushuhudiaji ili kufanikisha malengo manne ya utafiti: kuchunguza uhusiano uliopo baina ya fasihi na tafakuri tunduizi, kuchunguza hali halisi ya ufundishaji wa stadi ya tafakuri tunduizi katika madarasa ya lugha na fasihi, kubainisha mikakati ya ufundishaji wa stadi ya tafakuri tunduizi na kutoa mfano wa namna stadi ya tafakuri tunduizi inavyoweza kukuzwa kupitia fasihi. Nadharia ya Ujengaji ndiyo iliyoongoza hatua mbalimbali za utafiti ulioibua makala hii. Imebainika kuwa, kutokana na uhusiano wa karibu uliopo baina ya fasihi na tafakuri tunduizi, fasihi ni nyenzo mwafaka ya ukuzaji wa tafakuri tunduizi. Licha ya hivyo, katika madarasa ya fasihi na lugha, walimu wanakabiliwa na changamoto lukuki katika ukuzaji wa tafakuri tunduizi: kukosa uelewa wa kina kuhusu tafakuri tunduizi, kushindwa kujumuisha vema stadi ya tafakuri tunduizi katika masomo yao, na matumizi ya mbinu zisizo mwafaka. Zaidi ya hivyo, makala inabainisha sio tu mikakati mwafaka ya ukuzaji wa tafakuri tunduizi kupitia ufundishaji wa fasihi, bali pia inabainisha namna ambavyo fasihi inaweza kutumika*

*kukuza stadi ya tafakuri tunduizi kupitia mikakati tofauti ikiwemo ujifunzaji unaoegemea kwenye utatuzi wa tatizo.*

## 1.0 Utangulizi

Karne ya 21 inatawaliwa na mabadiliko ya haraka katika nyanja zote za maisha. Mabadiliko haya ya mara kwa mara yanahusiana na mahitaji ya karne hii, ambapo namna za kuishi na njia za kuwasiliana na watu wengine zimebadilika kwa kiasi kikubwa (Reynolds, na wenzake, 2017). Ili watu waweze kuendana na kasi ya mabadiliko na mahitaji ya karne ya 21, ni lazima wajifunze stadi zitakazowawezesha kukabiliana na hali ya maisha iliyopo (Saleh, 2019).

Stadi za Karne ya 21 hurejelewa kwa namna tofauti: Stadi zisizo za kiutambuzi, stadi laini, stadi nzima za ukuzaji mtoto, stadi zinazohamishika, stadi za maisha, stadi za kuhamasishwa, stadi za kijamii na kihisia, umilisi wa jumla na uwezo wa jumla (REB, 2015; *Global Partneship for Education*, 2020).

Binkley na wenzake (2010) wanaeleza kuwa stadi za Karne ya 21 ni uwezo na sifa zinazoweza kufundishwa ili kuendeleza namna ya kufikiria, kujifunza, kufanya kazi, na kuishi duniani. Aidha, kwa mujibu wa *Central Board of Secondry Education* (2020), stadi za Karne ya 21 ni uwezo unaohitajika kwa mtu binafsi ili aweze kuchangia katika maendeleo yake, jamii, taifa na kwa kiwango cha kimataifa.

Hivyo, stadi za Karne ya 21 ni pamoja na ubunifu na ugunduzi, tafakuri tunduizi, utatuzi wa matatizo, kufanya uamuzi, mawasiliano, ushirikiano, ujuzi wa kusoma na kuandika, ujuzi wa TEHAMA, uraia, stadi za kazi na wajibu wa kibinafsi na kijamii (Binkley na wenzake, 2010). Kaufman (2013) anasema kwamba ni lazima stadi hizi zijumuishwe katika kila somo pamoja na dhamira zake ili wanafunzi waweze kuwa na umahiri nazo. Maelezo ya mtaalamu huyu yanaonesha kwamba ili wanafunzi waweze kuwa na uimahiri na stadi za Karne ya 21, ni lazima ziingizwe katika mitaala ya kila somo. Aidha, baada ya kuwa na umahiri na stadi hizi,

wanafunzi wanatarajiwa kuwa na uwezo wa kushindana kwenye soko la ajira kitaifa na kimataifa. Hii pia ni njia mojawapo ya kuhusisha darasa na hali halisi ya maisha kwa kuwa zinatoa uwezo muhimu unaohitajika kwa mafanikio ya kikazi na kimaisha katika karne hii.

Ili kufanikisha haya, baadhi ya nchi duniani zilibadilisha mitaala yao ya elimu zikisisitiza mtaala unaoegemea katika uwezo. Mtaala huu unaweka mkazo katika ujifunzaji ulio hai unaokuza stadi ya tafakuri tunduizi (Reynolds na wenzake, 2017; Nsengimana, 2021). Mtaala unaoegemea katika uwezo pia unarejelewa kwa namna tofauti katika nchi mbalimbali. Kwa mfano, nchi ya Tanzania inatumia istilahi ya mtaala unaoegemea katika ujuzi. Huku nchini Rwanda, wanatumia istilahi ya mtaala unaoegemea katika uwezo. Kuna pia wanaotumia istilahi ya mtaala unaoegemea katika umilisi. Licha ya tofauti zilizopo katika istilahi hizi, zinamaanisha kitu kile kile kwa mazingira tofauti.

Tafiti zimebaini kuwa stadi ya tafakuri tunduizi inasaidia sio tu kumjenga mwanafunzi wa Karne ya 21 anayehitajika bali pia ni msingi muhimu wa stadi nyingine za Karne ya 21. Aidha, stadi hii husaidia katika ukuzaji wa stadi za lugha zinazomwezesha mwanafunzi kukuza umilisi wa kimawasiliano katika miktadha tofauti (Paul na Elder, 2006; Makame, 2019).

Hivyo, umilisi wa mawasiliano unahusu uelewa wa nini cha kusema kwa kuzingatia hali au muktadha uliopo, washiriki pamoja na makusudio yao kwa kutumia lugha inayostahili. Hii ina maana kwamba huwezi kukuza stadi za mawasiliano miongoni mwa wanafunzi pasipo kuwawezesha vema kuwa na stadi ya tafakuri tunduizi. Hivyo basi, ni jukumu la mwalimu wa fasihi kuwasaidia wanafunzi kukuza stadi za mawasiliano kadri wanavyoshughulika na kazi tofauti za kifasihi.

Aidha, kumekuwepo na madai kuwa, wanafunzi hasa wa vyuo vikuu hawana kiwango cha juu cha stadi ya tafakuri tunduizi kutokana na kwamba hawakupewa misingi mizuri ya kuendeleza stadi hii kuanzia shule za sekondari, na hivyo, kuweza kuathiri matokeo yao ya darasani na hata

kazini (Tung na Chang, 2009; Saleh, 2019). Hii ni bayana kwamba tatizo hili la stadi ya tafakuri tunduizi linajitokeza kwa wanafunzi wa vyuo vikuu na wale wa sekondari. Hapa ndipo kuna haja ya kuangalia namna ambavyo ufundishaji wa fasihi katika madarasa ya fasihi ya Kiswahili unaweza kukuza stadi ya tafakuri tunduizi miongoni mwa wanafunzi wa sekondari na hivyo kuwajengea misingi mizuri ya stadi hii hata watakapofika chuo kikuu.

Aidha, Tung na Chang (2009) wanatanabahisha kwamba stadi ya tafakuri tunduizi na fasihi vina uhusiano wa karibu. Wataalamu hawa wanaeleza pia kwamba usomaji wa kazi za kifasihi unakuza stadi za tafakuri tunduizi zinazomwezesha mwanafunzi kuhusisha anachokisoma na hali halisi ya maisha. Pamoja na hayo, maelezo haya mazuri yanatuachia swali juu ya namna gani hasa fasihi inaweza kutumika kukuza stadi ya tafakuri tunduizi. Kabla hatujajadili zaidi uhusiano uliopo baina ya fasihi na tafakuri tunduizi, ni muhimu kueleza kwa kifupi methodolojia na nadharia ya utafiti iliyofanikisha makala hii.

## 2.0 Methodolojia na Nadharia ya Utafiti

Data za utafiti ulioibua makala hii zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya uchanganuzi wa matini, ushuhudiaji pamoja na mahojiano. Ushuhudiaji wa somo darasani ulifanywa kwa shule nne teule. Mahojiano ya walimu wanne wa fasihi pia yalifanyika kwa shule hizo. Tulitumia misimbo tofauti ili kutofautisha data zilizokusanywa. Tulitumia A kuwakilisha mwalimu wa fasihi kwenye shule ya kwanza na B kuwalikisha mwalimu wa fasihi kwenye shule ya pili. Pia, C ilitumiwa kuwakilisha mwalimu wa fasihi kwenye shule ya tatu, na D ilitumiwa kuwakilisha mwalimu wa fasihi kwenye shule ya nne.

Kwa upande wa nadharia, licha ya tafiti tangulizi kuonekana kutumia nadharia tofauti kama vile Nadharia ya Utabia, Nadharia za Ujifunzaji wa Kijamii na Kiutambuzi, Nadharia ya Uendeleaji na Nadharia ya Ujengaji (Thompson, 2011; Mashaza, 2017), katika utafiti uliozaa makala hii, tuliona kwamba Nadharia ya Ujengaji ndiyo inafaa zaidi kuongoza ukusanyaji na uchambuzi wa data. Nadharia ya Ujengaji inafafanua namna ambavyo

binadamu hufikia kujua yale ajuayo. Hii ina maana kwamba ujifunzaji hauhusiki na kukariri maarifa tu bali huhusika na mchakato wa kujenga maarifa mapya kupitia kiwango cha juu cha stadi ya kufikiria. Kiwango hiki kinahusisha matendo kama vile kulinganisha, kutafsiri, kusanisi, kutathmini na kupata maarifa mapya kutokana na maarifa ya awali ambayo huwa nayo mjifunzaji (Boyanton, 2015 katika Mashaza, 2017).

Nadharia ya Ujengaji inashikilia kwamba, wanafunzi ndio kitovu cha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji (Singh na wenzake, 2020). Wanafunzi wanashirikishwa kikamilifu katika ujifunzaji hai unaowawezesha kupata maarifa tofauti kutokana na tajriba zao. Wakati huu wanafunzi wanagundua na kubadilisha taarifa za zamani ili zitumike katika mazingira mapya ya utatuzi wa tatizo. Hivyo, Nadharia ya Ujengaji inachukulia ujengaji wa maarifa na utatuzi wa tatizo kama moyo wa ujifunzaji (Mashaza, 2017).

## 3.0 Uhusiano wa Fasihi na Tafakuri Tunduizi

Gajdusek na Dommelen (1993) na Van (2009) kama wanavyorejelewa na Mohammad na wenzake (2011) wanasema kwamba fasihi na stadi ya tafakuri tunduizi vina uhusiano wa karibu. Kutokana na uhusiano huu, kuathiriana ni jambo lisiloepukika. Wataalamu hawa wanatanabahisha kwamba fasihi ni nyenzo muhimu ya kukuza tafakuri tunduizi miongoni mwa wanafunzi wa lugha. Aidha, Ghosn (2002) anatanabahisha kwamba, fasihi inaweza kuleta mabadiliko katika mitazamo ya wanafunzi. Hivyo basi, fasihi inawawezesha wanafunzi kutafakari kuhusu maisha yao, ujifunzaji wao na lugha yao au ile wanayoitumia (Langer, 1997).

Maelezo haya yanaonesha kwamba fasihi inawasaidia wanafunzi kujenga uwezo wao wa kufikiria kuhusu maisha yao na ya jamii yao kwa ujumla. Hivyo, fasihi huwasaidia wanafunzi wa lugha kukuza stadi ya tafakuri tunduizi kwa kuangalia yaliyomo katika jamii kwa jicho la kiuhakiki. Hili hujitokeza pale wanafunzi wanapoweza kuhusisha kile wanachokisoma katika kazi za kifasihi na maisha yao ya kila siku.

Kwa mfano, wanafunzi wanaweza kupewa kazi ya kusoma *Riwaya ya Watoto wa Maman'tilie* iliyoandikwa na Mbogo (2002*)*. Riwaya hii inaeleza maisha ya jamii tofauti za Kiafrika zinazoishi katika maisha duni kutokana na umaskini. Maisha haya huwafanya watoto waliozaliwa katika mazingira haya kukosa haki zao za msingi kama vile afya, malezi, lishe na haki nyinginezo. Hii huwafanya watoto hawa kuishi maisha ya kujitegemea na kujiingiza katika vitendo haramu kama vile: ulevi wa kupindukia, uuzaji wa dawa za kulevya, uwizi na vitendo vinginevyo ambavyo ni hatari kwa jamii. Matokeo ya vitendo hivi ni kuuawa na kuleta matatizo kwa familia ya watu wanaobaki. Licha ya matatizo haya, riwaya hii inaonesha kwamba bado akinamama wanapambana ili watunze familia zao.

Kupitia usomaji wa kazi hii, wanafunzi wanahusisha maisha ya wahusika tofauti wa riwaya hii na maisha yao wenyewe au maisha ya watu wanaoishi nao katika jamii. Wanafunzi wanaweza kujifunza tabia zinazopaswa kuigwa dhidi ya zile zinazopaswa kuepukwa. Kwa mfano, tabia ya Dani ya uwizi, na tabia ya Lomolomo ya ulevi kama tabia mbaya zinazopaswa kuepukwa na kila mwanajamii. Licha ya tabia hizi mbaya, kuna tabia za kuigwa kama vile tabia ya Maman'tilie aliyefanya juu chini ili kuitunza familia yake, mapenzi ya dhati ya Zenabu kwa watoto wa Maman'tilie na tabia nyinginezo zinazojitokeza katika riwaya hii.

Usomaji wa riwaya hii unawapa fursa wanafunzi kuhusisha tabia hizi na tabia zao wenyewe au za watu wanaoishi naoa katika jamii yao na hivyo kuamua nini kinapaswa kufanyika. Hii inajitokeza kupitia mijadala wanayoweza kufanya baada ya kusoma kazi husika wakiongozwa na mwalimu. Kadri wanafunzi wanavyojenga hoja kutokana na msimamo wao ndipo wanakuza stadi za tafakuri tunduizi ambazo ni kuchambua, kusanisi na kutathmini.

Tuchukuwe pia mfano wa pili wa *Tamthilia ya Wakati Ukuta* iliyotungwa na Hussein (1973*)*. Tamthilia hii inaeleza mgororo wa kizazi kipya na kizazi cha kale (vijana na watu wazima). Mgogoro huu unabainishwa kupitia msichana wa kisasa, Tatu na mzazi wake (Mama). Tatu alitaka kujistarehesha kama mtoto wa kisasa ila mama yake alimkataza. Siku moja

Tatu alikwenda pamoja na Swai katika sinema bila kukubaliana na mama yake. Matokeo yake, Tatu na Swai walifunga ndoa pasipo kupanga. Ndoa hii haikudumu kwa kuwa ilivunjika baada ya muda mfupi.

Kupitia usomaji au uigizaji wa tamthilia hii, wanafunzi wanaweza kuhusisha tabia za Swai na Tatu na tabia zao au za wenzao. Wanafunzi pia wanaweza kujadili madhara yaliyompata Tatu kutokana na kutofuata maelekezo ya mzazi wake. Matokeo yake ni kuolewa bila kupanga na ndoa kuvunjika. Zaidi ya ndoa kuvunjika, huenda Tatu aliweza kupata mimba au maradhi mengine ya kuambukizwa kama vile UKIMWI.

Hivyo basi, kutokana na matokeo ya tabia mbaya za Tatu na Swai kama zilivyodhihirishwa katika tamthilia hii, wanafunzi wanaweza kurekebisha tabia na kufuata maelekezo ya wazazi wao. Wanafunzi pia wanaweza kuwaonya wenzao wenye tabia zinazofanana na za wahusika wa tamthilia hii ili waweze kuzirekebisha. Ili wanafunzi waweze kutekeleza haya, wanatakiwa kuelewa, kuchambua, kusanisi na kutathmini taarifa walizozipata kutoka katika kazi ya fasihi wanayoisoma na kuzihusisha na maisha ya kila siku ya jamii yao. Hii itawasaidia kuelewa nini kinafaa na nini hakifai kufanyika kutokana na muktadha husika. Zaidi ya hayo, mwanafunzi atatumia maarifa aliyoyapata kutokana na kazi ya kifasihi aliyoisoma na kuyatumia katika utatuzi wa matatizo yanayoweza kumkabili katika siku zijazo. Hii huenda pamoja na mhimili wa Nadharia ya Ujengaji unaosisitiza kubadilisha maarifa ya zamani ili yatumike katika utatuzi wa tatizo lililopo au litakaloweza kujitokeza.

Tung na Chang (2009) wanathibitisha kwamba stadi ya tafakuri tunduizi na fasihi vina asili moja. Wataalamu hawa wanasema kwamba usomaji wa kazi za kifasihi unahitaji stadi ya tafakuri tunduizi ili kupata maana ya kazi inayokusudiwa. Hii ina maana kwamba ili msomaji wa kazi ya kifasihi apate maana inayokusudiwa katika kazi ya fasihi, anahitajika kuonesha uwezo wa kutafakari. Uwezo huo ni kama vile: kutofautisha ukweli kutoka katika maoni, kuwa na uelewa wa maana halisi ya kazi ya kifasihi na kile mwandishi anachotaka kumaanisha, kugundua sababu za kuwepo kwa tukio na kuhusisha kile msomaji anachokisoma na maisha halisi ya kila siku.

Ili msomaji wa kazi ya fasihi aweze kuonesha uwezo huo ni lazima apitie kwenye baadhi ya stadi za tafakuri tunduizi kama vile maelezo, uchambuzi, usanisi, tafsiri, tathmini, utatuzi wa matatizo, kuwa na hoja zenye mantiki na matumizi yake. Hivyo basi, ni rahisi sana kukuza stadi hizi za tafakuri tunduizi wakati wa ufundishaji wa fasihi.

Tuchukue pia mfano wa *Riwaya ya Watoto wa Maman'tilie*. Ili mwanafunzi aweze kutathmini na kuamua kwamba baadhi ya wahusika wa riwaya hii ni wazuri au wabaya, inamhitaji kuwa na vigezo vya kuaminika ili aweze kuthibitisha jibu lake.

Kwa mfano, mwanafunzi hawezi kusema kwamba Lomolomo alikuwa na tabia mbaya tu. Ili athibitishe haya, analazimika kutoa mifano inayoeleweka kutokana na kile ambacho amesoma. Aidha, mwanafunzi anaweza kutoa sababu kadhaa zinazowafanya wahusika tofauti kufanya wanavyofanya na matokeo ya matendo yao. Kwa mfano, kilichomchagiza Dani kwenda kuiba mali za watu na matokeo yake, nini matokeo ya ulevi wa Lomolomo, matokeo ya juhudi za Maman'tilie katika ujenzi wa familia, matokeo ya mwalimu Chikoya kuwatorosha wanafunzi shule na mengineyo.

Ili mwanafunzi aweze kufanikishaa haya, analazimika kupitia katika stadi za tafakuri tunduizi. Stadi hizi ni kama vile kueleza, kuchambua, kusanisi na kutathmini hoja/ taarifa mbadala kutokana na kile ambacho amesoma kabla ya kutoa hukumu au maoni yake kutokana tabia ya mhusika fulani. Hapo ndipo fasihi inapokuza stadi za tafakuri tunduizi.

Maelezo haya yanaonesha wazi kwamba fasihi na stadi za tafakuri tunduizi zina uhusiano wa karibu na haziwezi kutenganishwa. Hii ni kwa sababu kadri msomaji wa kazi za kifasihi anavyojishughulisha na kazi hizi, ndivyo anavyohusisha kile anachokisoma na maisha yake ya kila siku. Mwanafunzi anapata uelewa wa nini kinafaa au kisichofaa na hivyo kupata fursa ya kuona nini kinapaswa kufanyika baada ya kuelewa kuchambua, kusanisi na kutahmini taarifa anazozipata katika kazi za kifasihi anazozisoma.

## 4.0 Hali Halisi ya Ufundishaji wa Tafakuri Tunduizi katika Madarasa ya Lugha na Fasihi

Licha ya baadhi ya nchi duniani kubadilisha mitaala ya elimu ili kukuza stadi ya tafakuri tunduizi, bado kuna changamoto zinazokabili jitihada za ukuzaji wa stadi hii muhimu. Kabla hatujajadili changamoto hizi kwa kina na utatuzi wake, kwanza kuoneshe maoni ya walimu wa fasihi kuhusu mchango wa fasihi katika kukuza stadi ya tafakuri tunduizi kama tulivyobaini katika utafiti wetu. Mahojiano ya walimu wa fasihi yalionesha kwamba fasihi ina mchango mkubwa katika kukuza stadi ya tafakuri tunduizi. Mwalimu B alidhihirisha hilo kupitia dondoo lifuatalo:

> Fasihi inaweza kukuza stadi ya tafakuri tunduizi. Stadi ya tafakuri tunduizi inawasaidia wanafunzi kuhusisha kile wanachokisoma katika kazi ya fasihi na maisha yao kila siku. Kwa hiyo, wanafunzi wanaweza kuangalia kinachofaa na kisichofaa katika matendo yao na kuweza kurekebisha kutokana na kile jamii inahitaji (Mwalimu, B).

Dondoo hili linaonesha kwamba stadi ya tafakuri tunduizi inawasaidia wanafunzi kuhusisha kile wanachokisoma/wanachosikiliza katika kazi za kifasihi na maisha yao ya kila siku. Hii inawasaidia kuweza kurekebisha baadhi ya tabia zao zisizofaa. Hoja ya fasihi ya kukuza stadi ya tafakuri tunduizi pia iliungwa mkono na mwalimu wa fasihi kwenye shule B. Anasema:

> Fasihi inasaidia sana katika ukuzaji wa stadi ya tafakuri tunduizi. Hii ni kwa sababu fasihi ni kioo cha jamii ambacho mwanajamii hujiangalia na kuweza kuona wapi amesimama kutokana na kile jamii inahitaji. Zaidi ya hayo, fasihi inatoa fursa kwa wanajamii kuweza kujua kinachohitajika na kuisaidia jamii iweze kuwa nzuri zaidi. Ili mwanajamii aweze kuelewa haya na kutafuta suluhisho, ni lazima akuze stadi ya tafakuri tunduizi (Mwalimu,D).

Dondoo hili pia linaonesha kwamba fasihi ina mchango mkubwa wa kukuza stadi ya tafakuri tunduizi. Kutokana na aina ya kazi ya kifasihi anayoisoma mwanafunzi, inamsaidia kupata picha ya jamii anamoishi. Na hivyo anaweza kuona nini kinapaswa kufanyika ili kujenga jamii nzuri. Mwanafunzi anagundua haya kupitia stadi za tafakuri tunduizi ambazo ni kuchambua, kusanisi na kutathmini taarifa anazozitoa katika kazi ya fasihi anayoisoma.

Pamoja na maelezo haya mazuri, swali la kujiuliza ni je, walimu wanaijua stadi ya tafakuri tunduizi na namna inavyojumuishwa katika somo la fasihi? Data zilizokusanywa zilionesha kwamba kuna walimu wa fasihi ambao hawajui maana ya stadi ya tafakuri tunduizi. Mfano mmojawapo ni mwalimu wa fasihi katika shule C aliyekiri kutojua. Aidha, walimu wengine pia wanaonekana kutoielewa stadi ya tafakuri tunduizi kwa ukamilifu wake. Mmoja miongoni mwao alifasili stadi ya tafakuri tunduizi kama ifuatavyo:

> Ni mambo yanayoweza kujitokeza katika somo ambayo unaweza kuwa umeyatarajia au hukuyatarajia. Mambo haya yanaweza kujitokeza darasani katika ufundishaji au ujifunzaji wa somo fulani. Na mambo haya ni muhimu katika maisha ya kila siku ya wanafunzi na jamii kwa ujumla (Mwalimu, D).

Dondoo hili linaonesha kwamba mwalimu huyu anaiona stadi ya tafakuri tunduizi kama mambo yanayoweza kuja ghafla katika somo, yaani bila mpango wowote. Hii ina maana kwamba, kwa mtazamo potofu, walimu hawalazimiki kujumuisha stadi ya tafakuri tunduizi katika somo wanaloliandaa, kwani tafakuri tunduizi inaweza kujitokeza katika somo hata pasipo kupangwa. Tatizo hili la kutojua kwa ukamilifu maana ya stadi ya tafakuri tunduizi halikujitokeza kwa mwalimu huyu pekee. Mwalimu mwenzake anaifasili stadi ya tafakuri tunduizi kama ifuatavyo:

> Tafakuri tunduizi ni mfumo au mbinu inayotumiwa katika ufundishaji. Mwalimu anawapa wanafunzi kazi tofauti na kutafakari ili waweze kutambua jambo fulani analowapa. Kwa mfano, mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi maana

> ya tamthilia. Unapowauliza maana ya tamthilia, unaweza kuwapanga katika makundi wakatafakari kwa kina kwa kutafuta maana ya kina kuhusu tamthilia (Mwalimu, A).

Mwalimu wa pili anaiona stadi ya tafakuri tunduizi kama mbinu ya ufundishaji inayotumiwa na mwalimu katika somo fulani. Maelezo ya mwalimu huyu si sahihi kwa sababu stadi hii haihusiani na mbinu ya ufundishaji bali ni stadi inayoweza kukuzwa kupitia utumizi wa mbinu tofauti za ufundishaji. Madondoo haya mawili yanaonesha wazi kwamba walimu hawaelewi kwa ukamilifu maana ya stadi ya tafakuri tunduizi.

Hivyo, maarifa haya ya walimu kuhusu stadi ya tafakuri tunduizi huathiri ufundishaji na tathmini ya stadi hii. Data zinathibitisha kwamba, walimu wa fasihi hawajumuishi vilivyo stadi ya tafakuri tunduizi katika andalio la somo. Stadi hii inajitokeza katika sehemu ya uwezo wa jumla katika masomo wanayoyaandaa. Hivyo, stadi za tafakuri tunduizi hazionekani kuwepo miongoni mwa stadi zinazopaswa kukuzwa katika somo la fasihi. Huu ni mfano wa andalio la somo la fasihi lililoandaliwa na mwalimu wa fasihi katika shule ya B:

| | |
|---|---|
| **Aina ya wanafunzi wenye mahitaji maalum ya kielimu watakao shughulikiwa katika somo,idadi yao kulingana na mahitaji yao** | Hakuna |
| **Mada** | Fasihi katika Kiswahili |
| **Uwezo uhitajiwao katika somo** | Ufafanuzi na Uainishaji wa tanzu za fasihi na pamoja na utoaji wa mifano ya kila aina. |
| **Somo lenyewe** | **Dhima ya Sanaa ya fasihi katika jamii** |
| **Malengo ya kujifunza** | Baaada ya somo hili, wanafunzi wataweza kufafanua na kueleza mifano ya matumizi na dhima ya fasihi katika jamii |
| **Mahali ambapo somo litapofundishiwa** | Darasani |
| **Vifaa au zana kwa wanafunzi wote** | Chaki, ubao, kalamu, vitabu , picha na kadhalika |
| **Vitabu vya rejea** | Kitabu cha mwanafunzi wa lugha Kiswahili kidato cha 4 REB |

| **Muda na hatua** | **Mbinu za kufundishia na kujifunzia**<br>Ushirikishaji na mazungumzo ya wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili | | **Tafakuri tunduizi na maswala mtambuka vielezewe+maelezo mafupi** |
|---|---|---|---|
| | **Wajibu wa mwalimu** | **Wajibu wa mwanafunzi** | |
| **Utangulizi**<br>Dakika 5 | Maamkizi<br>Mwalimu atawauliza wanafunzi kufafanua tanzu za fasihi. | Wanafunzi watafafanua fasihi simulizi na fasihi andishi katika makundi mawili wakiongozwa na walimu. | -Adabu<br>Ukuzajikifra |
| **Somo lenyewe**<br>Dakika 30 | Mwalimu atawaongoza wanafunzi na kuwashirikisha katika kujadili dhima ya fasihi katika jamii.<br>Mfano:<br>Kuelimisha jamii<br>Kuburudisha jamii<br>Kukuza uwezo wa kufikiri | Wanafunzi watashirikiana katika kujadili dhima ya fasihi katika jammi wakiongozwa na mwalimu.<br><br>Watatofautisha fasihi simulizi na fasihi wakiongozwa na mwalimu. | -Ushirikiano<br>-Ukuzajikifra<br>-Mwenendo wa kuheshimiana |
| **Hitimisho**<br>Dakika 5 | Kuwapa wanafunzi zoezi la kujadili umuhimu wa fasihi katika shule za Rwanda. | Wanafunzi watashirikiana kufanya zoezi la kujadili umuhimu wa fasihi katika shule za Rwanda. | -Ushirikiana<br><br>-Ukuzaji fikra |
| **Tathmini ya mwalimu** | Some somo limefundishwa vizuri na wanafunzi wamefaulu kazi asilimia 90% | | |


**Kielelezo (1):** Mfano wa Andalio la Somo la Fasihi Lililoandaliwa na Mwalimu wa Fasihi katika Shule ya B

Mfano huu wa andalio la somo unaonesha wazi kwamba stadi ya tafakuri tunduizi inajitokeza katika nafasi ya uwezo wa jumla. Matokeo yake ni kuwa stadi ya tafakuri tunduizi haitekelezwi vilivyo katika somo la fasihi. Mwalimu huyu amejaribu kutafuta istilahi "*Ukuzaji Fikra*" kwa kumaanisha stadi ya tafakuri tunduizi ilhali tafakuri tunduizi ni stadi ambayo ina istilahi yake mahususi. Stadi hii pia inapaswa kukuzwa kama stadi nyingine.

Kutojumuisha stadi ya tafakuri tunduizi katika somo kunawafanya walimu wa fasihi kutoifundisha na kuitathmini vilivyo katika kazi tofauti za ufundishaji na ujifunzaji zinazotolewa kwa wanafunzi. Data za ushuhudiaji darasani zinaonesha kwamba walimu wanatumia vitenzi vya ngazi ya chini wanapowauliza wanafunzi maswali ya ujifunzaji. Haya ni baadhi ya

maswali wanayoulizwa wanafunzi kuhusu somo lenye anwani: "*Umuhimu wa Nyimbo*" kwenye shule A. Eleza maana ya wimbo, taja aina za nyimbo, tofautisha nyimbo na mashairi, bainisha umuhimu wa nyimbo. Haya ni maswali yanayoweza kumsaidia mwanafunzi kukumbuka na kuonyesha uelewa wake kuhusu nyimbo na umuhimu wake. Kwa mtazamo wetu, tunaona kuwa kunapaswa kuongezwa maswali tofauti yanayoweza kuwawezesha wanafunzi kuona nyimbo kama njia mojawapo ya kujitatulia matatizo ikiwa ni pamoja na kujiajiri. Wanafunzi wangeweza hata kupewa kazi kadhaa za utungaji wa nyimbo.

Licha ya data za ushuhudiaji darasani, matokeo ya uchambuzi wa nyaraka za walimu pia yanaonesha kwamba walimu wa fasihi hawatathmini vilivyo stadi ya tafakuri tunduizi katika mitihani. Huu ni mfano wa mtihani wa muhula wa kwanza (2021) uliotolewa kwa wanafunzi wa kidato cha sita katika mchepuo wa lugha (*Literature in English*, Kinyarwanda na Kiswahili: LKK) kwenye shule B:



SEHEMU B: FASIHI /Alama /50

Chagua maswali matano katika sehemu hii

2. a)Eleza maana ya tamthilia uku ukitoa mifano ya majina mawili ya tamthilia ulizosoma darasani?/alama 5

b)Taja sifa bainifu tano za utanzu wa tamthilia./alama5

3.a) eleza maana ya ushairi kisha utaje jina la mshairi mojawapo wa washairi wa kiswahiliunayemujua pamoja na shairi aliloliandika./alama5

b)eleza sifa 5 za utanzu wa ushairi /alama 5

4. Jadili tofauti zozote tano baina ya utanzu wa riwaya na tamthilia./alama10

5. Jadili sifa tano bainifu za utanzu wa riwaya. /alama 10

6. Eleza umuhimu wa Methali katika jamii huku ukitoa na kueleza mifano tatuya methali za Kiswahili ulizosoma darasani./alama10

7. Eleza tofauti zilizopo kati ya riwaya na hadithi fupi./alama10

**Kielelezo (2):** Mfano wa Mtihani kwa Wanafunzi wa Kidato cha sita

Kama inavyoonekana, maswali ya mtihani huu yanawasaidia wanafunzi kukumbuka na kuonesha nini wanaelewa kuhusu fasihi tu kama maarifa waliyofundishwa darasani. Maswali haya hayawapi wanafunzi fursa ya kukuza stadi za tafakuri tunduizi. Stadi hizi ni kama vile kusanisi, kuchambua na kutathmini hoja kutoka katika kazi za kifasihi walizozisoma ili kujibu maswali husika. Ikumbukwe kwamba wanafunzi wanapaswa kutumia maarifa wanayojifunza darasani katika mazingira ya utatuzi wa

matatizo. Mhimili mmojawapo wa Nadharia ya Ujengaji unaeleza kwamba wanafunzi wanasaidiwa kujenga maarifa wanayojifunza katika utatuzi wa tatizo. Hii ina maana kwamba kazi yoyote ya fasihi inayotolewa kwa wanafunzi inapaswa kuwasaidia wanafunzi kutatua matatizo kwa kutumia maarifa ya awali waliyojifunza darasani.

Tanujaya (2016) kama anavyorejelewa na Singh na wenzake (2020) anaeleza kwamba walimu wanashindwa kujumuisha stadi za tafakuri tunduizi katika masomo yao kwa sababu hawana uwezo wa kuwa wabunifu na kutumia mbinu mpya wakati wa ufundishaji. Aidha, Abdul-Aziz (2017) akirejelewa na Singh na wenzake (2020), anasema kwamba ujumuishaji wa tafakuri tunduizi katika somo lolote unahitaji mambo kadhaa kama vile mpango, maandalizi, vifaa na hata mafunzo kwa walimu.

Hivyo basi, mafunzo kwa walimu wa fasihi yanahitajika ili yawasaidie kuifundisha na kuitathmini stadi ya tafakuri tunduizi kwa usahihi. Mafunzo haya ni muhimu kwa sababu walimu wengi wakiwemo wa fasihi hawakujifunza katika mazingira yanayowasaidia kukuza stadi ya tafakuri tunduizi.

Pili, hakuna programu zinazowasaidia walimu kujifunza zaidi kuhusu tafakuri tunduizi na mwisho, hakuna mwongozo kwa walimu wa lugha kuhusu jinsi wanavyoweza kutekeleza stadi ya tafakuri tunduizi (Buskist na Irins, 2008; Singh na wenzake, 2020).

Data za ushuhudiaji zilionesha kwamba kuna idadi kubwa ya wanafunzi darasani kwenye baadhi ya shule. Idadi hii inawazuia walimu wa fasihi kutumia mikakati ya ufundishaji inayofaa katika ukuzaji wa stadi ya tafakuri tunduizi. Mmojawapo wa walimu wa fasihi anathibitisha hili kama ifuatavyo:

> Kuna changamoto ambayo ni msongamano wa wanafunzi darasani/ wingi wa wanafunzi darasani. Darasa lenye wanafunzi 50 siyo rahisi kuwafundisha na kuwapa kazi za tathmini endelezi kwa kuwa ni wengi. Unaweza hata kukosa

> muda wa kusoma na kusahihisha kazi zao kutokona na uwingi wao (Mwalimu, A).

Singh (2018) kama anavyorejelewa na Singh na wenzake (2020) anasema kwamba walimu wengi hawaelewi mbinu faafu zinazotumiwa kufundisha tafakuri tunduizi kwa darasa lenye wanafunzi wengi. Mara nyingi mwalimu anatumia mbinu ya mhadhara na matumizi ya kazi za makundi ili kurahisisha kazi hata kama wanafunzi hawajaelewa somo linahusu nini.

Mojawapo wa mihimili ya Nadharia ya Ujengaji inaeleza kwamba mwanafunzi anapaswa kuwa kitovu cha ujifunzaji wakati mwalimu anakuwa muwezeshaji. Utumizi wa njia ya mhadhara inampa mamlaka yote mwalimu kuonekana kama ndiye anajua yote. Mwanafunzi anaangaliwa kama debe tubu linalopaswa kujazwa. Hivyo basi, njia ya mhadhara haimsaidii mwanafunzi chochote katika ujifunzaji kwa sababu haimshirikishi katika mchakato wenyewe wa ujifunzaji.

Data zilizokusanywa zilionesha pia kwamba walimu wa fasihi hawana vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi kukuza stadi ya tafakuri tunduizi. Shida hii inatibitishwa na mmoja wa walimu wa fasihi anaposema:

> Changamoto nyingine ni uhaba wa vitabu/zana za ufundishaji. Kwa mfano unapotaka kufundisha usomaji wa hadithi au usomaji wa riwaya, ni shida kubwa kupata kazi za kifasihi zinazoweza kukusaidia katika mchakato huo. Kazi za kifasihi zinazokuwepo ni chache sana ukilinganisha na idadi ya wanafunzi. Zaidi ya hapo, ni kazi za zamani. Kazi nyingi haziendani na karne hii (Mwalimu, C).

Nukuu za mtoa taarifa huyu zinaonesha kwamba walimu wa fasihi wanakumbana na tatizo kubwa la ukosefu wa kazi za kifasihi zinazoweza kutumiwa kufundishia fasihi. Hii inatokana na idadi ya wanafunzi waliomo darasani. Aidha, kazi chache zilizopo ni za zamani sana ikilinganishwa na muktadha halisi wa ufundishaji. Changamoto ya ukosefu wa vifaa vya ufundishaji iliungwa mkono na mwalimu wa fasihi katika shule B. mwalimu

huyu alisema kwamba licha ya kukosekana kwa kazi za kifasihi, hakuna pia vifaa vya teknolojia vinavyowawezesha walimu na wanafunzi kujifunza. Mwalimu huyu alidhihirisha changamoto hii kwa kusema:

> Jambo jingine ni uhaba wa vifaa vya kiteknolojia. Kwa mfano, unapotaka kufundisha hotuba, ni lazima kuwa na redio, simu, spika au komputa. Ila tunapofundisha hayo, tunakosa vifaa hivyo. Unakosa kifaa cha kutumia ili ufundishe kazi ya kifasihi kupitia mfano wa kazi husika. Kwa mfano, unapotaka kufundisha hotuba, unakosa jinsi unavyoweza kuwasaidia wanafunzi kusikia sauti ya kiongozi fulani anayehutubia taifa(Mwalimu, B).

Nukuu za watoa taarifa hawa zinaonesha kwamba ni kazi ngumu kufundisha baadhi ya vipera vya fasihi andishi na hata simulizi kama vile hadithi, hotuba, nyimbo na mashairi usipokuwa na vifaa vinavyoweza kukusaidia. Hivyo basi, mwalimu hafundishi vipera hivyo kwa usahihi kama mtaala unavyoagiza kuhusu matumizi ya vifaa husika.

Baholano (2017), kama alivyorejelewa na Khalid na wenzake (2021) anabainisha kwamba uwepo wa vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji ikiwemo Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ni mojawapo ya masharti ya kutekeleza stadi ya tafakuri tunduizi na kuendeleza ujifunzaji shirikishi. Mtaalamu huyu anamaanisha kwamba vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyoambatanishwa na teknolojia vinamsaidia mwanafunzi kutumia kile anachojifunza darasani katika utatuzi wa tatizo linaloweza kumkabili kimaisha. Hii pia inaendana na mhimili wa Nadharai ya Ujengaji unaotazama ujifunzaji shirikishi kama moyo wa ujifunzaji. Vifaa hivi vya ujifunzaji huwamotisha na kuwashirikisha wanafunzi katika somo husika. Na hivyo huwasaidia wanafunzi kujenga maarifa yao wenyewe yanayohitajika katika utatuzi wa tatizo lililopo (Mashaza, 2017).

## 5.0 Mikakati ya Kufundisha Stadi ya Tafakuri Tunduizi

Ukuzaji wa tafakuri tunduizi huenda pamoja na baadhi ya mikakati kadhaa ya ufundishaji (Radulović na Stančić, 2017). Bates (2015; Singh na wenzake,2020) wamebainisha mikakati kadhaa inayofaa kuweza kutumiwa hata katika ufundishaji wa fasihi kwa minajili ya kukuza stadi ya tafakuri tunduizi. Mikakati inayobainishwa na wataalamu hawa ni pamoja na ujifunzaji unaoegemea kwenye utatuzi wa tatizo, ujifunzaji unaoegemea kwenye uvumbuzi, ujifunzaji unaoegemea kwenye uchunguzi na ujifunzaji unaoegemea kwenye mradi.

Kutokana na changamoto zilizobainishwa na walengwa wetu wa utafiti, tuliona kwamba mikakati hii inaweza kufaa katika utatuzi wa changamoto zilizobainishwa kulingana na mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji yaliyopo. Hivyo basi, katika darasa la fasihi, mikakati hii inaweza kutekelezwa kwa kuiambatanisha na kazi tofauti za kifasihi. Kwa hivyo, katika mjadala ufuatao tutajadili kila mkakati na namna mwalimu anavyoweza kuutekeleza anapofundisha fasihi.

Kwanza ni ujifunzaji unaoegemea kwenye utatuzi wa tatizo. Huu ni mkabala wa ufundishaji ambapo ujifunzji huanza na tatizo linalopaswa kutatuliwa. Tatizo hilo linaweza kuhusiana na maisha halisi au tatizo alilokutana nalo mhusika fulani katika kazi ya kifasihi. Kutokana na tatizo hilo, wanafunzi wanaweza kuwekwa katika makundi na kujadili tatizo husika ili kuibuka na majibu tofauti baada ya kuchambua muktadha wa tatizo husika (Singh na Wenzake., 2020).

Kupitia makundi, wanafunzi hukaa pamoja na kutambua kile wanachojua, wanachohitaji kuelewa, jinsi na wapi wanaweza kupata taarifa mbalimbali

zinazowasaidia kutatua tatizo husika. Hivyo basi, mwalimu wa fasihi anaweza kuwashirikisha wanafunzi katika kazi za utatuzi wa tatizo analokutana nalo mhusika fulani katika kazi ya kifasihi wanayoisoma. Baada ya hapo, wanafunzi hukaa pamoja katika makundi yao kwa kushiriki maarifa, stadi, hoja na hata tajriba ili kubaini mikakati inayoweza kutumiwa ili kutatua tatizo husika (REB, 2015).

Makundi yanapaswa kuundwa kwa namna ambayo kila mwanakikundi atakuwa na kazi mahsusi ya kutekeleza kwa ukamilifu badala ya mwanafunzi mmoja tu katika kundi kufanya kazi yote peke yake kwa niaba ya kundi. Hivyo basi, wanafunzi katika makundi wanalazimika kugawana majukumu ili waweze kukamilisha kazi wanayopewa.

Hili pia linaendana na mhimili wa Nadharia ya Ujengaji ambao unaweka mkazo kwenye ujifunzaji shirikishi unaomwezesha mwanafunzi kushirikiana na wenzake kujenga maarifa yanayohusu utatuzi wa tatizo. Wanafunzi hawa wanashirikiana katika ujengaji wa maarifa yanayowasaidia kutatua tatizo husika. Mara nyingi maarifa haya yanajengwa kutokana na tajriba zao au maarifa tofauti waliyokuwa nayo kuhusu somo wanalojifunza.

Kwa mfano, mwalimu anaweza kuwashirikisha wanafunzi kusoma *Riwaya ya Watoto wa Maman'tilie*. Baada ya kusoma riwaya hii, wanafunzi wanaweza kupewa maswali tofauti ya kujadili katika makundi yao kisha wakaibuka na suluhisho. Maswali wanayoweza kupewa ni kama yafuatayo: A) Jadili madhara ya watoto kufukuzwa shule na athari zake kwao na jamii kwa ujumla. Toa mifano kutoka kazi uliyoisoma ukihusisha na maisha ya jamii yako. B) Unakubaliana na tabia ya Lomolomo ya ulevi? Nini madhara

ya ulevi katika maisha ya jamii kiuchumi? Nini kifanyike ili watu waepuke na tabia hii. C) Kutokana na riwaya unayoisoma, nini kinaweza kufanyika ili tuweze kuwa na familia yenye ushirikiano? Baada ya kufanya mjadala katika makundi yao, wanafunzi wanaweza kutakiwa kuwasilisha matokeo yao mbele ya hadhira na kuweza kujibu baadhi ya maswali wanayoulizwa.

Pili ni ujifunzaji unaoegemea kwenye uvumbuzi. Huu ni ujifunzaji unaowashirikisha wanafunzi katika ujifunzaji hai. Wanafunzi wanatakiwa kuchunguza mazingira kwa kuulizana maswali tofauti na kuweza kujibu maswali hayo kwa kutumia mawazo yao wenyewe. Wanafunzi ndio hutawala kila kitu, mwalimu anafanya kazi ya kuwaongoza au kuwasaidia wanafunzi.

Mwalimu wa fasihi anaweza kuwashirikisha wanafunzi katika usomaji au usikilizaji wa kazi ya kifasihi kisha wanafunzi wakajigawa katika makundi ili kuulizana maswali tofauti kuhusu kazi waliyoisoma au kusikiliza. Katika zoezi kama hili, mwalimu anapaswa kutoa mwongozo wa maswali wanayopaswa kuuulizwa wanafunzi ili wasiende nje ya muktadha wa kazi.

Maswali wanayopaswa kuulizana wanafunzi na kujibu yanapaswa kuendana na kazi wanayoisoma. Aidha, maswali haya yanapaswa kuwa shirikishi kiasi cha kuwachochea wanafunzi kutoa mawazo yao wenyewe.

Kwa mfano, wanafunzi wanaweza kuulizwa maswali yanayofanana na haya: A) Kazi unayoisoma/unayosikiliza inahusu nini? B) Anwani ya kazi hiyo inahusianaje na yaliyomo? C) Jadili sababu za kuipenda au kuichukia kazi unayoisoma. D) Ni sehemu ipi ya kazi unayoipenda zaidi na kwa nini? E) Ni mhusika yupi unayempenda au unayemchukia na kwa nini? F) Tabia za

mhusika …zinakufundisha nini katika maisha yako ya kila siku? G) Kama ingekuwa wewe ni mmoja wa wahusika wa kazi hii, ungefanya nini tofauti na mhusika husika? Kwa nini? H) Mwandishi anataka kutoa ujumbe (funzo) gani wakati wa kuandika kazi hii? Ujumbe unahusianaje na maisha yako na jamii yako kwa ujumla? I) Kutokana na ujumbe uliopata katika kazi uliyoisoma, unaenda kufanya nini tofauti na jinsi ulivyofanya? Wakati wa kufanya kazi hizi, mwalimu anapaswa kuwaongoza wanafunzi na kuwasaidia wanapokutana na changamoto.

Tatu ni ujifunzaji unaoegemea kwenye uchunguzi wa kesi. Katika ujifunzaji huu, mwalimu anawashirikisha wanafunzi katika majadiliano yenye lengo la kuwasaidia kujitegemea (Maming, 2018 katika Singh na wenzake., 2020). Uchunguzi wa kesi unalenga kuuliza maswali na kuwashirikisha wanafunzi kutafsiri maarifa kwa ajili ya kupata hitimisho lenye maantiki. Kwa hiyo, ujifunzaji unaoegemea katika uchunguzi wa kesi, unawasaidia wanafunzi kukuza stadi tofauti kwa kuchanganua na kutafakari matukio tofauti ya kimaisha kama yanavyojitokeza katika kazi za kifasihi. Kwa maneno mengine, uchunguzi wa kesi unawasaidia wanafunzi kuhusisha kile wanachosoma katika kazi za kifasihi na maisha yao ya kila siku. Hii inawapa wanafunzi fursa ya kuweza kuchangia katika uchunguzi wa tatizo na utatuzi wake.

Ujifunzaji unaoegemea katika uchunguzi, unawahitaji wanafunzi kuwa na maarifa ya awali yanayowasaidia kuchanganua kesi. Kwa hivyo, ni muhimu kwa wanafunzi kuwa na maarifa fulani kuhusu kile kinachojitokeza katika kazi ya kifasihi ili kuweza kutambua kesi husika. Kisha, wataweza kuihusisha na kile kinachojitokeza katika jamii na kuweza kuichunguza.

Hivyo basi, mwanafunzi anapaswa kusoma kazi ya kifasihi na kuielewa ili aweze kugundua kesi inayopaswa kufanyiwa uchunguzi.

Kwa mfano, wanafunzi wanaweza kushirikishwa katika usomaji wa *Riwaya ya Vipuli vya Figo*, kisha wakashirikishwa kufanya uchunguzi kutokana na kesi tofauti zinazojitokeza katika riwaya hii. Haya ni baadhi ya maswali ambayo wanafunzi wanaweza kushiriki kuyajibu. A) Kesi husika inayojitokeza katika kazi unayoisoma ni ipi? B) Kesi husika umeijuaje? Thibitisha jibu lako kwa mifano inayoeleweka. C) Ni ushahidi upi unaoonesha kwamba kesi fulani ipo? D) Nini madhara ya kesi husika kwa wanajamii? E) Tuseme kwamba ulikuwa mkuu wa Mji wa Daluta, nini ungefanya kutokana na kesi ya mauaji iliyopo? F) Kama polisi, kesi hii ya watu kupotea pasipo sababu kujulikana ungeifanyia kazi namna gani?

Kazi za uchunguzi wa kesi zinawasaidia wanafunzi kuhusisha mazingira ya darasa na kile kinachoweza kujitokeza katika jamii. Zaidi ya hayo, wanafunzi hupata uelewa wa jinsi wanavyoweza kushughulika na kesi hiyo au kesi inayofafana na hiyo inapotokea. Kwa maneno mengine, kazi za uchunguzi wa kesi zinamsaidia mwanafunzi kutatua baadhi ya matatizo yanayoweza kujitokeza katika jamii. Hii pia inaendana na mmojawapo wa mhimili wa Nadharia ya Ujengaji usemao kwamba utatuzi wa tatizo ni moyo wa ujifunzaji.

Mwisho ni ujifunzaji unaoegemea katika mradi. Katika ujifunzaji huu wanafunzi wanapewa kazi za kibinafsi au za makundi kwa kipindi fulani cha wakati. Mwalimu anawashirikisha wanafunzi kuchagua mada tofauti na kuzifanyia kazi. Wanafunzi wana uhuru wa kupanga kazi yao wenyewe, kuamua jinsi watakavyoifanya, kipindi gani wataifanya kazi husika,

majukumu ya kila mmoja katika ukamilishaji wa kazi na nyenzo zitakazotumiwa kuikamilisha kazi. Kazi mradi zinaweka msingi wake katika ulimwengu halisi ambao unawashirikisha wanafunzi kuwajibika katika kazi za ujifunzaji (Bates, 2015). Baadhi ya kazi hizi ni kama vile utungaji wa kazi za kifasihi kama hadithi fupi, riwaya, mashairi, nyimbo, tamthilia na kazi nyinginezo.

Utungaji wa kazi kama hizi unaweza kuwa suluhisho la ukosefu wa kazi za kifasihi zinazotumiwa katika ufundishaji na ujifunzaji. Kazi hizi zilizotungwa na wanafunzi zinaweza kuhaririwa na kutumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi. Zaidi hayo, ni njia mojawapo inayoweza kuwasaidia wanafunzi kuanza mchakato wa kijiajiri kutokana na kazi wanazozitunga.

Pamoja na mikakati tuliyoijadili, ni lazima mwalimu afanye maandalizi mapema kabla ya kuwasilisha somo lake darasani.

Aidha, mwalimu anapaswa kuleta mifano halisi ya tafakuri tunduizi kutoka katika maisha ya kila siku. Mifano hii inapaswa kuwa ni ile ambayo mwalimu ameikusanya kabla ya kuanza muhula au kadri muhula unavyoendelea. Mifano hii halisi itawasaidia wanafunzi kupata stadi zitakazowawezesha kuwa karibu na kile wanachokisoma, wanachosikisia, wanachoona au uzoefu wanaoupata katika maisha yao. Zaidi ya hapo, mifano halisi inawasaidia wanafunzi kuhusisha kile wanachojifunza na maisha yao ya kila siku ya utatuzi wa matatizo. Hii ni kwa kuwa, baadhi ya matatizo hayo yanajitokeza katika mifano wanayoitoa. Aidha, mwalimu anapaswa kuhakikisha kuwa mifano halisi anayoitoa inahusiana na somo lake (Buskist na Irins, 2008).

Ukuzaji wa stadi za tafakuri tunduizi haupaswi kuishia katika mazoezi pekee. Stadi ya tafakuri tunduizi inapaswa kutathminiwa pia kupitia

mitihani, majaribio na kazi nyingine za tathmini. Katika ujengaji wa tathmini hizi, mwalimu anapaswa kuwauliza maswali wazi yanayowataka wanafunzi kutoa hoja zao wenyewe. Maswali haya pia yanapaswa kuhusiana na muktadha wa hali halisi ya utatuzi wa tatizo ambapo wanafunzi wanapaswa kupiga hatua zaidi ya kile walichojifunza darasani. Maswali haya yanapaswa kuwa na jibu zaidi ya moja na kumwezesha mwanafunzi kutoa hoja mbadala kutetea jibu lake (Lai, 2009). Baada ya kuona mikakati inayofaa kutumiwa kufundisha tafakuri tunduizi, tunajielekeza katika kujadili namna ambavyo fasihi inaweza kutumika kukuza stadi ya tafakuri tunduizi.

## 6.0 Ukuzaji wa Stadi ya Tafakuri Tunduizi kupitia Fasihi

Glaserfeld (1995) kama anavyorejelewa na Mohammad na Nima (2013), anaeleza kwamba elimu ina malengo makuu mawili yanayotarajiwa. Malengo hayo ni kwanza kuwawezesha wanafunzi kufikiria wenyewe na pili ni kuendeleza njia za kufikiria kwa kizazi kijacho. Maelezo haya yanaonesha kwamba elimu haipaswi kujihusisha kwa upekee na utoaji maarifa tu kiasi cha wanafunzi kuchukuliwa kama madebe matupu yanayopaswa kujazwa, huku mwalimu akiwa kitovu cha ufundishaji na ujifunzaji. Badala yake, elimu inapaswa kujishughulisha na namna wanafunzi wanavyopaswa kuyatekeleza maarifa wanayojifunza au kuyatengeneza katika maisha yao ya kila siku. Hili linaweza kufanyika kwa kuwashirikisha wanafunzi katika utatuzi wa matatizo yanayohitaji utumiaji wa stadi za tafakuri tunduizi.

Bean (1996) kama anavyorejelewa na Iakovos (2011) anasema kwamba tafakuri tunduizi ni stadi ambayo wanafunzi wanaweza kujifunza darasani. Kwa hiyo, kuna uwezekano wa fasihi kutumika kukuza stadi ya tafakuri tunduizi kutokana na uhusiano wa karibu kati ya dhana hizi. Katika ufundishaji wa tafakuri tunduizi, mwalimu anapaswa kutia mkazo kwenye maeneo mawili: Kwanza, ni masuala ya somo kama vile mikakati ya kutoa maswali kwa wanafunzi, maingiliano ya wanafunzi, mrejesho wa mwalimu au wanafunzi kuhusu kazi zilizofanywa wanafunzi. Pili, ni eneo la maudhui ya somo yanayokuza stadi ya tafakuri tunduizi (Li, 2018).

Maelezo haya yanamaanisha kwamba mwalimu wa fasihi anapotaka kufundisha stadi ya tafakuri tunduizi katika somo la fasihi, ni lazima aandae maswali yanayoendana na malengo na maudhui ya somo anayotarajia kufundisha. Hii inatokana na ukweli kwamba si kila aina ya swali linaweza kukuza stadi ya tafakuri tunduizi. Licha ya hayo, mwalimu anapaswa kutoa mrejesho kwa kile wanachokifanya wanafunzi. Hii itawasaidia wanafunzi kuona nini wamefanya vizuri na kipi hawakufanya vizuri. Aidha, mrejesho lazima uoneshe namna gani wanafunzi wangeweza kufanya vizuri zaidi. Kwa mfano, mwalimu anaweza kutoa kazi ya kifasihi ya kusoma/ kusikiliza. Baada ya kusomwa na wanafunzi, anaweza kuwauliza maswali tofauti kama vile:

a) Kazi unayoisoma/ unayoisikiliza inahusu nini?

b) Jadili sababu za kuipenda au kuichukia kazi husika;

c) Ipi ni sehemu ya kazi unayoipenda zaidi na kwa nini?

d) Kazi husika ya fasihi ina funzo gani na unawezaje kuihusiha na maisha yako ya kila siku?

e) Je, unakubaliana na mwenendo wa mhusika? Kama ndio kwa nini na kama hapana ni kwa nini?

f) Kama ingekuwa wewe ndio mhusika wa kazi hii ya fasihi, ungefanya nini tofauti na mhusika husika?

g) Ungetakiwa kuiendeleza hadithi husika, ungeiendeleza namna gani?

Wakati wa kujibu maswali haya, inafaa mwalimu awape wanafunzi muda wa kutosha ili waweze kufikiria kwa kina kuhusu maswali kabla ya kuyatolea majibu. Wakati wa kujibu maswali haya, wanafunzi wanakuza stadi za tafakuri tunduizi na stadi nyingine za maisha. Stadi hizi ni kama vile stadi ya ubunifu na ugunduzi, utatuzi wa matatizo na mawasiliano. Kwa hakika, stadi hizi zote zinaitegemea sana stadi ya tafakuri tunduizi.

## 7.0 Hitimisho

Katika makala hii tumebainisha kwa uwazi namna fasihi inavyoweza kutumika katika ukuzaji wa stadi ya tafakuri tunduizi. Katika mjadala huu tumeonesha uhusiano wa karibu uliopo kati ya fasihi na tafakuri tunduizi. Kabla ya kuonesha hili, makala imejadili kwa kina sababu za msingi za kufundisha stadi hii kwa wanafunzi wa Karne ya 21. Yote haya yamefanyika kwanza kuonesha ni kwa namna gani stadi ya tafakuri tunduizi ni ya muhimu sana katika maisha yetu.

Baada ya hapo, makala hii imeonesha baadhi ya changamoto mbalimbali zinazowakabili walimu wa fasihi katika ukuzaji wa tafakuri tunduizi katika madarasa ya lugha. Pamoja na hayo makala hii imebainisha baadhi ya mikakati inayoweza kutumiwa na walimu wa fasili ili kukabiliana na changamoto zilizobainishwa kadri serikali inavyoshughulika na uendelezaji wa sekta ya elimu.

Hivyo basi, inaonekana wazi kwamba fasihi inafaa sana katika ukuzaji wa tafakuri tunduizi. Ila kunahitajika ushirikiano mkubwa baina ya walimu wa fasihi wa sekondari, vyuo vya ualimu, vyuo vikuu na hata viongozi wa serikali. Ushirikiano huu utafanikisha upatikanaji wa kazi nyingi za kifasihi na vifaa vya kiteknolojia vinazoweza kutumiwa wakati wa ufundishaji wa fasihi unaoweza kukuza tafakuri tunduizi. Aidha, ni lazima pia walimu wa fasihi kupewa mafunzo ya mara kwa mara kuhusu ufundishaji na tathmini ya tafakuri tunduizi. Mafunzo haya yatawawezesha kufundisha na kuitathmini vilivyo stadi ya tafakuri tunduizi licha ya changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika madarasa ya lugha na fasihi katika shule za sekondari.

**Marejeleo**

Bates, A., W. (2015). *Teaching in Digital Age: Guidelines for Designing Teaching and Learning.* Vancouver: Tony Bates Associated LTD

Binkley, M., Erstad, O., Herman, J., Raizen, S., Ripley, M., & Rumble, M. (2010). *Assessment and Teaching of 21st Century Skills project draft White Paper:* Chuo Kikuu cha Merbourne.

Buskist, W. & Irons, G.J. (2008). *Simple Strategies for Teaching your Students to Think Critically*. Katika D. S. Dunn, J. S. Halonen, na R. A. Smith (Wahariri), Teaching critical thinking in psychology: AH and book of best practices. UK: Blackwell Publishing Ltd.

Central Board of Secondry Education. (2020). *21st Century Skills: A Hand Book*. Delhi: The Secretary Central of Secondry Education.

Ghosn, I. (2002). Four good reasons to use Literature in primary school ELT. *ELT Journal, 2*(56), 172-179.

Global Partnership for Education. (2020). *21st Century Skills: What potential role for the Global Partnership for Education? A Landscape Review*: Global Partnership for Education

Hussein, N. E. (1973). *Wakati Ukuta.* Nairobi: East African Publishing House.

Iakovos, T. (2011). Critical and creative thinking in the English language classroom. *International Journal of Humanities and Social Science, 1*(8), 82-86.

Kaufman, J. K. (2013). 21 ways to 21st Century skills: Why students need them and ideas for practical implementation. *Kappa Delta Pi Record, 9*(2), 78-83. Doi: 10.1080/00228958.2013.786594.

Khalid, L., Bucheerei, J., & Issah, M. (2021). Pre-service teachers' perceptions of barriers to promoting critical thinking skills in the classroom. *SAGE Open*,1-9. Doi.org/10.1177/2158244021103609.

Lai, Y., K. (2009). Assessing students' critical thinking performance: Urging for measurements using multi-response format. *Journal of Thinking Skills and Creativity, 4*(1), 70-76. Doi.org/10.1016/j.tsc.2009.02.001.

Langer, J. (1997). Literacy acquisition through Literature. *Journal of Adolescent and Adult Literacy, 40*, 602-614.

Li, L. (2018). Thinking skills and creativity in second language education: Where are we now? *Journal Thinking Skills and Creativity*. Doi.org/10.1016/j.tsc.2016.11.005. Kutoka http://hdl.handle.net/10871/33700.

Makame, K. O. (2019). Mkabala wa kimawasiliano katika ufundishaji wa lugha ya pili: Mifano kutoka ufundishaji wa Kiswahili kwa wageni Tanzania. *African Journals onLine (OJOL),82*(1), 72-85.

Mashaza, L. G. (2017). Theoretical perspectives on critical thinking teaching: Reflections from field experiences from a Norwegian lower secondary school in comparison to Tanzanian secondary school teaching practices. *Journal of Education and Learning, 11*(3), 312-318.

Mbogo, E. (1996). *Vipuli vya Figo.* Nairobi: East African Educational Publishers

Mbogo, E. (2002). *Watoto wa Maman'tilie.* Dar es Salaam: Heko Publishers.

Mohammad, K. & Nima, S. (2013). Literature stance in developing critical thinking: A pedagogical look. *International Journal of Research Studies in Language Learning, 2*(4), 101-108. DOI: 10.5861/ijrsll.2012.154.

Mohammad, K., Rezaei, S., & Derakhshan, A. (2011). Literature in EFL/ESL classroom.*English Language Teaching, , 4*(1), 201-208. Doi: 10.5539/elt. v4n1p201.

Nsengimana, V. (2021). Implementation of competence-based curriculum in Rwanda: Opportunities and challenges. *Rwandan Journal of Education, 5*(1), 129-138.

Paul, R., & Elder, L. (2006). *The Miniature Guide to Critical Thinking Concepts and Tools*. (Toleo la 4). Tomales, CA: The Foundation for Critical Thinking.

Radulović, L. & Stančić, M. (2017). What is needed to develop critical thinking in schools? *C E P* S *Journal*, *7*(3), 9-25.

REB. (2015). *Competence Based Curriculum: Curriculum Framework Pre-Primary to Upper Secondary*. Kigali: REB.

Reynolds, R. Taveres, N. & Notari, M. (2017). 21st Century skills and global education roadmaps. *ResearchGate*, *7*(17), 1-14. Doi: 10.1007/978-981-10-2481-8-2

Rezaei, S., Derakhshan, A., Bagherkazemi, M. (2011). Critical thinking in language education. *Journal of Language Teaching and Research*, *2*(4), 769-777. Doi:10.4304/jltr.2.4.769-777.

Saleh, E. S. (2019). Critical thinking as a 21st Century skill: Conceptions, implementation and challenges in the EFL classroom. *European Journal of Foreign Language Teaching*, *4*(1)1- 16. Doi: 10.5281/zenodo.2542838.

Singh, C. K. S., Singh, T.S.M., Ja'afar, H., Tek, o., Kaur, H., Mostafa, N & Yunung, M. (2020). Teaching strategies to develop higher order thinking skills in English literature. *International Journal of Innovation, Creativity and Change*, *11(*8), 211-231.

Thompson, C. (2011). Critical Thinking across the curriculum: Process over output. *International Journal of Humanities and Social Science,1* (9), 1-7.

Tung, C. A., & Chang, S. Y. (2009). Developing critical thinking through Literature reading. *Feng Chia Journal of Humanities and Social Sciences*, *19* (1), 287-317.